Kwanza ni vizuri kufahamu kuwa hakuna jambo lolote linaloshindikana hapa duniani,  lakini habari mbaya ni kuwa yapo mambo mengi yanayotushinda sisi wanadamu, na hiyo ni kutokana na kuwa kwa namna moja au nyingine tumekosa kujua njia sahihi ya kutatua matatizo hayo au wakati mwingine kukosa maarifa ya kutosha juu ya tatizo husika, kwa mfano watu wawili wanaweza kuumwa Malaria lakini mmoja akawa na ufahamu kuwa huu ni ugonjwa wa malaria, hivyo akaenda hospitali akapewa dawa akanywa akapona, na mwingine kwa kuwa hajawahi kufahamu au kusikia juu ya ugonjwa huo akadhani amelogwa akaenda kwa mganga, akaambiwa leta unyayo wa jirani yako, lakini mwisho wa siku akajikuta anakufa katika hali ile  ile, hiyo ni kwasababu alikosa maarifa ya kujua chanzo cha tatizo na njia sahihi  ya kulitatua..

Vivyo hivyo na magonjwa mengine yote yasiyotibika, kama vile ukimwi, kansa, Kisukari n.k. sio kwamba hayana tiba, hapana tiba yanayo ukimwi unatibika isipokuwa tu tumekosa maarifa ya kutosha ya kujua mahali pa kuyatatua na njia sahihi,..Na hiyo imetufanya tuhangaike huku na huko na mwisho wa siku tunaangamia…Madaktari wetu wanafanya kazi njema ya Mungu, lakini upo wakati ambao uwezo wao kutibu unafika kikomo, hivyo inahitaji mtu mwingine ambaye mwenye uwezo mkubwa zaidi ya yeye kukusaidia hapo.

Habari  njema ni kuwa yupo anayeweza kuyaondoa yote pasipo gharama yoyote na huyo si mwingine zaidi ya YESU KRISTO. Zipo shuhuda nyingi, na bado zitaendelea kuwa nyingi za watu wanaoponywa magonjwa hayo kwa damu yake. Anachotaka kwako sio tu kukuponya mwili wako lakini pia kuiponya roho yako, kwasababu hiyo ndiyo ya muhimu zaidi.

Kwani kuna makundi mawili ya watu wanaopatwa na matatizo haya, kundi la kwanza ni wale waliopata kutokana na dhambi zao, kwamfano mtu amekuwa mzinzi na mwasherati matokeo yake akapata Ukimwi, sasa watu wengi wa namna hii wakati mwingine wanataka Mungu awaponye, lakini hawezi kuwaponya kama hawatakuwa tayari kutubu na kuacha dhambi zao, kundi la pili, ni wale wanaopatwa kwa njia za kawaida tu sio kwa dhambi, sasa hawa kama mtu atakuwa bado yupo nje ya Kristo ni vizuri akaokoka na kama yupo ndani ya Kristo asiwe na wasiwasi Bwana atamponya tu.

Jambo ni moja tu ni kumwamini Bwana YESU..Kwasababu ndiye pekee aliyekufa kwa ajili yetu, hakuna kiongozi yoyote, au mtume yeyote, au nabii yeyote ambaye aliyewahi kuyatoa maisha yake makamilifu kwa ajili ya shida za watu wengine, hakuna haijawahi kutokea katika historia na wala haitakaa itokee, Ni mmoja tu ambaye ni YESU KRISTO. Yeye ndiye aliyeyachukua magonjwa yetu yote na madhaifu yetu.

> *Mathayo 8:16 "Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi,*
>
> *17 ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu."*
>
> *Isaya 53:4 Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa.*
>
> *5 Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.*

Wewe Unajuaje kuwa ni huyo huyo **YESU** ndiye aliyekupitisha katika ukurasa huu?, Ameona shida zako na magonjwa yako unayopitia kuwa muda mrefu, Hivyo usiogope leo hii ugonjwa huo utaondoka, Jambo la kwanza unalopaswa kufanya kama hajatubu basi tubu leo hapo ulipo kwa kumaanisha kabisa kuacha dhambi zako na kumwishia yeye, kwasababu hapo ulipo anakuona, na anakutazama, anajua kila kitu

kilichopo ndani ya moyo wako, hivyo tubu makosa yako yote kwa kumaanisha ikiwa upo nje ya Kristo, na yeye atakusamehe, kisha baada ya maombi ambayo nitaomba na wewe muda si mrefu, ukatafute mahali wanapobatiza ubatizo sahihi wa kuzamishwa katika maji mengi na kwa jina la YESU KRISTO ili ukamilishe wokovu wako, na baada ya hapo Mungu mwenyewe atakupa kipawa cha Roho Mtakatifu.

Sasa nataka ufanya jambo moja hapo ulipo weka mkono wako wa kuume mahali pale unapoumwa,..kama ni mwili mzima au ndani ya damu weka mkono wako katika kifua chako.. Kisha Sema kwa sauti maneno haya kwa **IMANI.**

**BWANA YESU, NAJA KWAKO, NINAKIRI KUWA WEWE NI BWANA NA MWOKOZI WA MAISHA YANGU, NA TENA WEWE NI MPONYAJI WANGU, WALA SINA MPONYAJI MWINGINE ILA WEWE, UMEWAPONYA WENGI NA SHUHUDA ZAO KILA SIKU NINAZISIKIA NA KUZIONA MBELE YA MACHO YA WATU, NAMI LEO HII NATAKA UNIPONYE NA MIMI EE YESU MPENZI, NIMEONA KUWA HAKUNA MWINGINE ANGEWEZA KUNIPENDA KAMA WEWE ULIVYONIPENDA, KWA KUJITOA NAFSI YAKO, MAISHA YAKO, NA UHAI WAKO ILI MIMI NIPATE UKOMBOZI WA BURE, NA LEO HII NINAKIRI KUWA SITAKUACHA, NITATEMBEA NA WEWE SIKU ZOTE ZA MAISHA YANGU.**

**ASANTE BWANA YESU KWA KUNIPONYA.**

**AMEN.**

Ikiwa umefuatiliza sala hiyo, sasa hapo ulipo jiangalie mahali ulipokuwa unaumwa, au nenda hospitali kapime, na huo ugonjwa ulionao utakuta umeshaondoka. Hivyo usiache kututumia shuhuda zako kwa namba hizi:

**+255789001312**

**+255654555788,**

Au kwa barua pepe hii:

email: **watakatifuwasikuzamwisho@gmail.com**

Pia unaweza soma shuhuda mbalimbali hapo chini zitakazokusaidia kujenga imani yako kwa Bwana.

---

**Mada Nyinginezo:**

**USHUHUDA WA UPONYAJI WA UKIMWI.**

**USHUHUDA WA UPONYAJI WA KANSA.**

**NAMNA GANI NITAPOKEA NGUVU ZA BWANA YESU?**

**YESU MPONYAJI.**

**JE! NI KWELI BWANA ALIMAANISHA HATUTAONJA MAUTI KABISA TUKIMWAMINI?(YOHANA 11:25)**

**UNYAKUO.**

---

**Rudi Nyumbani:**

Share on:
WhatsApp

Print this post